

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA, MHESHIMIWA BALOZI KHAMIS
MUSSA OMAR (Mb) KATIKA MAHAFALI YA 15 YA BODI YA
WATAALAMU WA UNUNUZI NA UGAVI (PSPTB), TAREHE 23
OKTOBA 2026, UKUMBI WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE
(JNICC), DAR ES SALAAM**

Ndugu Jacob Jail Kibona, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya PSPTB;

Ndugu Alex J. Haraba, Kaimu Kamishna wa Sera za Ununuzi wa Umma, Wizara ya Fedha;

Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya PSPTB;

Ndugu Godfred B. Mbanyi, Mkurugenzi Mtendaji wa PSPTB;

Viongozi wa Serikali na wawakilishi wa taasisi za umma na binafsi;

Wakurugenzi na watumishi wa PSPTB;

Wataalam wa mnyororo wa ugavi;

Wahitimu, wazazi na walezi;

Wageni waalikwa, wanahabari, mabibi na mabwana.

Itifaki imezingatiwa.

Ndugu Mwenyekiti, viongozi na wageni waalikwa, wahitimu, mabibi na mabwana,

Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya na kutuwezesha kukutana katika Mahafali ya 15 ya Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB). Ninawasilisha salamu za **Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Balizi Khamis Mussa Omar (Mb)**, ambaye **amenituma kumwakilisha** kutokana na majukumu mengine ya kitaifa. Kwa niaba yake, ninawapongeza PSPTB kwa kuandaa mahafali haya na kwa kuendelea kusimamia maendeleo ya taaluma ya mnyororo wa ugavi nchini.

Ndugu Mwenyekiti,

Ninawapongeza **wahitimu 583** wanaotunukiwa vyeti katika mahafali haya. Kati yao, **11** wamehitimu Stashahada ya Kitaaluma ya Ununuzi na Ugavi (Professional Diploma in Procurement and Supply), **64** wamehitimu ngazi ya Shahada ya Kitaaluma (Graduate Professional in Procurement and Supply), **453** wamehitimu Shahada ya Juu ya Kitaaluma (Certified Procurement and Supply Professional (CPSP-T)), na **55** wamekamilisha mafunzo maalumu ya ukaguzi wa mnyororo wa ugavi. Mafanikio haya yanaongeza idadi ya wataalamu wanaohitajika katika upangaji, ununuzi, usimamizi wa mikataba, ugavi na ukaguzi.

Ndugu wahitimu,

Vyeti hivi vinaambatana na wajibu wa kutekeleza majukumu kwa uadilifu, weledi na uwajibikaji. Kama tunavyofahamu, Serikali imetunga Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi ya Mwaka 2025 ili kuunganisha na kuimarisha usimamizi wa shughuli zinazohusiana na mnyororo wa ugavi zikiwemo: ununuzi, ugomboaji na uondoshaji wa mizigo, upokeaji, uhifadhi,

matumizi, usambazaji na uondoshaji wa mali. Katika hatua zote, zingatieni Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410, udhibiti wa gharama, zuieni upotevu, na hakikisheni Serikali inapata thamani halisi ya fedha.

Ndugu Mwenyekiti,

Utekelezaji wa sera na sheria unahitaji wataalamu wenye ujuzi, uadilifu na uwezo wa kufanya maamuzi kwa maslahi ya umma. Ninawahimiza wahitimu kutumia maarifa yao kwa weledi, kuendelea kujifunza na kuzingatia viwango vya maadili ya taaluma. Taasisi na waajiri nao wanapaswa kuunga mkono maendeleo ya kitaaluma na kuhakikisha kuwa majukumu yanatekelezwa na watu wenye sifa zinazostahili.

Aidha, uwajibikaji unahitaji udhibiti wa ndani unaofanya kazi, kumbukumbu sahihi, ufuatiliaji wa mikataba na utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi. Rushwa, udanganyifu, mgongano wa maslahi na matumizi mabaya ya mali za umma hudhoofisha ushindani na kuondoa thamani ya fedha; vitendo hivyo havipaswi kuvumiliwa.

Ndugu Mwenyekiti,

Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi unahitaji ushirikiano wa Wizara na taasisi zote zinazohusika, mamlaka za udhibiti, taasisi za umma, sekta binafsi na taasisi za elimu na mafunzo. Kila mdau atekeleze wajibu wake na kuhakikisha kuwa shughuli za mnyororo wa ugavi zinafuatiliwa kwa kutumia taarifa zinazopimika. Tathmini ya utekelezaji izingatie ufanisi, gharama, upatikanaji wa bidhaa na huduma, usimamizi wa mali na thamani halisi ya fedha.

Ninaitaka PSPTB kuendelea kuchangia katika kuimarisha weledi wa taaluma kwa kuzingatia jukumu lake la kisheria, na kushirikiana na wadau

ili uwezo wa wataalamu uendane na mwelekeo wa sera na mahitaji ya nchi. Kwa upande mwingine, taasisi zote zinazohusika zinapaswa kutekeleza sera na sheria kwa vitendo na kuwajibika kwa matokeo.

Ndugu Mwenyekiti,

Ninahimiza PSPTB kuendelea kushirikiana na vyuo vya elimu ya juu na waajiri ili wahitimu wa programu za mnyororo wa ugavi waelewe umuhimu wa kufanya mitihani ya kitaaluma na kukamilisha usajili unaostahili. Bodi iendeele kuboresha mitaala na mafunzo ili yaendane na mahitaji ya kazi, mabadiliko ya sheria na matumizi ya teknolojia. Wataalamu nao washiriki katika mafunzo endelevu na kutimiza wajibu wao wa usajili na ada za kitaaluma kwa mujibu wa taratibu.

Ndugu Mwenyekiti,

Ninatoa wito kwa waajiri wa sekta ya umma na binafsi kuhakikisha kuwa nafasi za ununuzi na ugavi zinajazwa na watumishi wenye sifa stahiki na wanaotimiza masharti ya usajili yanayotakiwa. PSPTB, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi husika, iendeele kutoa elimu na kufuatilia uzingatiaji wa matakwa ya kitaaluma na miundo ya utumishi. Masuala ya madaraja na maslahi ya watumishi yashughulikiwe kupitia taratibu za Serikali zinazohusika.

Ndugu Mwenyekiti,

Ninapongeza kuanzishwa kwa mafunzo maalumu ya ukaguzi wa mnyororo wa ugavi. Ujuzi huu unaweza kuimarisha uwezo wa taasisi kutambua mapungufu, kujibu hoja za ukaguzi kwa wakati na kutekeleza mapendekezo ya wakaguzi. Naihimiza PSPTB kuimarisha ushirikiano na Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Ofisi ya Taifa ya

Ukaguzi (NAOT), Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali (IAG), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), kwa kuzingatia majukumu ya kila taasisi. Waajiri wahakikishe watumishi wanaohusika wanapata nafasi ya kushiriki mafunzo hayo.

Ndugu Mwenyekiti,

Uunganishaji wa Mfumo wa Usajili wa PSPTB (ORS) na Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST) unapaswa kusaidia kuhakiki sifa za kitaaluma za wanaoshiriki katika shughuli za mnyororo wa ugavi. Kwa hiyo, ninawahimiza PSPTB na PPRA kushirikiana kufanya tathmini ya pamoja ya mifumo hiyo, kubaini changamoto za kiutendaji na kuweka hatua za kuzitatua. Tathmini hiyo izingatie ufanisi wa ubadilishanaji wa taarifa na namna mifumo inavyosaidia uzingatiaji wa sheria na taratibu.

Ndugu Mwenyekiti,

Serikali inatambua mchango wa wataalamu wa mnyororo wa ugavi katika kulinda rasilimali za umma na kuboresha utoaji wa huduma. Masuala yanayohusu utambuzi wa sifa za kitaaluma na stahiki za watumishi yataendelea kushughulikiwa kwa kushirikiana na mamlaka husika na kwa kuzingatia sheria, miundo ya utumishi na taratibu zilizowekwa.

Ndugu Mwenyekiti,

Ninaitaka PSPTB kuendelea kusimamia maadili ya taaluma, kuchukua hatua pale ukiukaji unapothibitishwa na kuwahimiza wataalamu kutunza hadhi ya taaluma yao. Aidha, Bodi iendeele kuboresha huduma za usajili na mafunzo, na kutumia rasilimali zilizopo kwa kuzingatia vipaumbele

vyake. Ushirikiano wa Serikali, waajiri, vyuo na sekta binafsi ni muhimu katika kuhakikisha taaluma inakidhi mahitaji ya sasa na yajayo.

Ndugu wahitimu,

Ninawapongeza kwa hatua mliyofikia. Endeleeni kujifunza, kuzingatia maadili na kutumia ujuzi wenu kutatua changamoto za taasisi zenu. Mafanikio yenu yatapimwa pia kwa namna mtakavyosaidia kuimarisha uwazi, ushindani, uwajibikaji na matumizi bora ya rasilimali za umma.

Ndugu Mwenyekiti, viongozi na wageni waalikwa,

Kwa mara nyingine, ninawapongeza wahitimu wote na kuishukuru PSPTB kwa kazi yake ya kuendeleza taaluma ya ununuzi na ugavi. Sasa nitakabidhi vyeti na zawadi kwa wahitimu kama ilivyopangwa katika ratiba ya mahafali haya.

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA.